> “Katika kiti cha enzi cha Daudi na ufalme wake; kuuthibitisha na kuutegemeza kwa **hukumu na kwa haki,** tangu sasa na hata milele.”
> Isaya 7:9



# seekingjusticetogether

LATEST NEWS & UPDATES

INTERNATIONAL SOCIAL JUSTICE COMMISSION

INTERNATIONAL SOCIAL JUSTICE COMMISSION

## Ya sasa



**Tume ya Kimataifa ya Maadili na maswala ya Jamii walikutana kwa mkutano wa ana kwa ana kwa mara ya kwanza kule** Sunbury Court London kabla ya janga kubwa. Tume ilizungumzia kuhusu mitindo ya maswala ya maadili na jamii. Mkutano huo ulihudhuriwa na wajumbe wa Tume ya Kimataifa ya Haki za Jamii (ISJC), Kanali **(Dr) Wendy Swan kama Mwenyekiti, na Dr Laurelle Smith kama Mwandishi.**

Oktoba, **Mafunzo ya namna ya kukabiliana na Utumwa wa kileo na Usafirishaji Haramu wa Binadamu yalifanyika** Nigeria na yaliwezeshwa na mjumbe wa Tume ya kimataifa ya haki za jamii**, Joy Ime-Sunday,** akiwa na **Meneja wa Kimataifa wa Mipango kutoka Teritori ya Uingereza na Ireland, Toluwanimi Jaiyebo, na Mratibu wa Kanda ya Africa (MSHTR), Anne Makumi.** Washiriki walijifunza kuhusu kazi za Jeshi la Wokovu katika kukabiliana na Utumwa wa kileo na Usafirishaji Haramu wa Binadamu na wakaweka sahihi zao kwenye kadi ya ahadi wakiashiria kujitoa kwao katika kikao chao kupambana na Utumwa wa kileo na Usafirishaji Haramu wa Binadamu (UKUHB) katika jamii zao.




## Tarehe kwa ajili ya Kalenda yako

- **Siku ya Haki za binadamu** - 10 Desemba
- **Siku ya Kimataifa ya Wakimbizi** - 18 Desemba
- **Siku ya Elimu ya Umoja wa Mataifa** - 24 Januari
- **Siku ya Haki ya Jamii Duniani** - 20 Februari
- **Siku ya Kimataifa ya Wanawake** - 8 Machi
- **Siku ya Kimataifa ya Kuondoa Ubaguzi** - 21 Machi
- **Siku ya Maji Duniani** - 22 Machi


# Majibu ya Utumwa wa Kileo na Usafirishaji Haramu wa Binadamu




## Data za kusaidia kuvuruga Usafirishaji


Jeshi la Wokovu limefurahishwa kupokea mapendekezo ya “Njia za kushirikiana kuvuruga” kama sehemu ya Data za kuzuia Usafirishaji tuzo ya 2022. Tukio hili lilisherehekea ushirika, mashirika na miradi inayotumia data na ufundi katika njia asilia ili kuwashirikisha wengine habari na kubadilisha mazingira ambamo usafirishaji na unyonyaji unashamiri.

**Mchango wa Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa**
Timu ya Kimataifa ya Jeshi la Wokovu ya Utumwa wa Kileo na Usafirishaji Haramu wa Binadamu imekuwa moja ya wabia sita ambao mchango wao ulijumuishwa katika ripoti iliyopelekwa kwenye Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Ripoti hii ilizingatia Usafirishaji wa watu katika mazingira ya Mabadiliko ya Hali ya Hewa na ilitolewa na mtaalamu maalum, Siobhan Mullally. Inaweza kupatikana hapa: https://owncloud.unog.ch/s/kFQa8RmZP4mS-Gn9?path=%2F2)%20Other%20Stakeholders#pdfviewer




# Tume ya Kimataifa ya Haki za Jamii na Umoja wa Mataifa

## Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa



Kikao cha 77 cha Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa kilifunguliwa tarehe 13 Septemba. Mikutano ya ngazi ya juu ilifanyika kutoka tarehe 20 hadi 26 Septemba na mihutasari ya mikutano yote na nyaraka za mitandaoni vinaweza kupatikana katika mtandao wa Umoja wa Mataifa https://press.un.org/en/content/general-assembly

## Siku ya Kimataifa ya Msichana

Siku ya Kimataifa ya Msichana ilifanyika tarehe 9 Oktoba na ilitoa sauti za wasichana wadogo waumini wa Jeshi la Wokovu duniani. Tukio hili la wote kuona lilitoa uwanja kwa wasichana kuonyesha karama zao - kusherehekea kwa ubunifu miaka 10 ya jitihada za wasichana. Tizama ukurasa wa mtandaoni ujionee yaliyotokea! https://salvationarmy.org/isjc/IDG2022







## Ipe Dunia rangi ya Chungwa

Siku 16 za Jitihada Dhidi ya Unyanyasaji wa wanawake zilianza tarehe 25 Novemba na zikaendelea hadi tarehe 10 Desemba Mwaka huu. Kiini cha mwaka kilikuwa “TUUNGANE”! kukomesha maonevu dhidi ya akina mama na wasichana: Tembelea mtandao wa chungwa upate misaada: https://www.salvationarmy.org/isjc/16Days

# Kutoka kwenye meza ya Wakurugenzi




*Hapo mwanzo kulikuwapo Neno, na Neno alikuwapo kwa Mungu, na Neno lilikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwapo kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakukufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza halikuiweza. Palikuwepo mtu, ametumwa kutoka kwa Mungu, jina lake Yohana. Huyo alikuja kwa ushuhuda, ili aishuhudie ile nuru, wote wapate kuamini kwa yeye.*

*Huyo hakuwa ile nuru, bali alikuja ili aishuhudie ile nuru. Kulikuwako nuru halisi, amtiaye nuru kila mtu, akija katika ulimwengu. Alikuwapo ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuja kwake, wala wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli.*

*Yohana 1:1-14*

Sawa na sheria za binadamu haikufikirika kwamba Mtakatifu Muumba kamwe angeweza kuwa mwanadamu. Ilikuwa Mungu abakie kuwa Mungu, katika umbo mwanadamu alimwona Mungu kuwa – mwenye nguvu, mkali na mwenye kuhukumu – na hata katika hali – Mungu aliishi juu ya mbingu, mbali na mwenye uwezo, mwenye kuogopwa na kusujudiwa, akiwa wazi anatofautishwa na mwanadamu na uumbaji.

Wazo kwamba Mungu angeweza kutambulika, angeweza kuonekana, "kuzaliwa" katika umasikini katika mji mdogo katika familia ya wakimbizi na kwamba angedhihirisha maisha ya upendo na huduma ya kujitoa kwa wengine na angeleta mashitaka kwa matajiri na wenye nguvu, ilikuwa haifikiriki katika karne ya kwanza ya Yuda. Katika uthibitisho katika dibaji ya injili ya Yohana kwamba "Neno likawa mwili", mvutano kati ya kushindwa kwa binadamu na Mungu kumeongezeka. Lakini hapa Mungu hakomi kuwa mkamilifu kuhusu mwili; Mungu huyu anachagua kuishi ndani ya mwili wa mwanadamu naye ni Yesu Kristo.

Mawazo ya kufikiria –
- Mungu hafanyi utetezi kutoka mbali lakini anakuja karibu katika mtu aitwaye Yesu Kristo.
- Utetezi na kupinga haki kwa niaba ya, na matakwa mengine mawili – uaminifu kwa utu wetu wenyewe na ulioelezwa na Yesu kwa mfano wake mwenyewe.
- Injili haiko nyuma kati ya yale yanayohusu hamu yetu ya kuwa sahihi; inapenda kuona yaliyosahihi yanafanywa.

Tunapojiandaa kusherehekea "Mungu pamoja nasi" msimu huu wa Krismasi, hebu tusiwasahau masikini na wasio na makao kwasababu ilikuwa kati yao ndiko Mtoto Kristo alichagua kuishi.

*Ian and Wendy Swan*
Makanali
Wakurugenzi – Tume ya Kimataifa ya Haki za Jamii

# Mambo ya Kuombea




Kwa wote wanusurika wa utumwa wa kileo na usafirishaji haramu wa binadamu na wale wanaopambana na kazi ya kutoa majibu, ili wapate mpenyo wa rasilimali za kiroho na kimwili wanazohitaji, na wapewe nguvu za kuendelea na mapambano.



Kwao viongozi duniani na wale wanaotengeneza maamuzi ya sera, hasa katika Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa, kwamba wazingatie hamu ya jamii zilizotengwa na wakomeshe ukosefu wa haki wa aina zote.

Mwisho upatikane wa mashambulizi dhidi ya wanawake na kwamba hili lipatikane kupitia njia za sera, jamii na tamaduni. Tunaomba nguvu za ziada wapewe wale ambao sasa hivi wamo, au wanusurika wa ukatili wa majumbani, wapate haki na amani wanayoistahili.





Amani na umoja upatikane katika maeneo ya ulimwengu yaliyokumbwa na vurugu. Tunapokaribia kipindi cha Krismasi, tunatafakari kuhusu wema wa Mungu na amani tuliyo nayo ndani yake. Tunaomba kwamba msimu huu wa siku kuu, amani hii itawafikia watu duniani.

# Rasilimali

